

KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL CENTRE

TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA:

NAFASI:

WAHUDUMU WA HUDUMA KWA WATEJA (CUSTOMER CARE):

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya kanda ya Kaskazini KCMC unapenda kuwatangazia nafasi za kujitolea katika Dawati la Huduma kwa Wateja.

Majukumu ya Kazi:

1. Kuwapokea na kuwaelekeza wagonjwa na wageni kwa heshima, ukarimu na weledi.
2. Kutoa taarifa sahihi kuhusu huduma, vitengo na taratibu za hospitali.
3. Kuwaelekeza wagonjwa na wageni kwenye maeneo au vitengo husika.
4. Kupokea na kushughulikia malalamiko, maoni na changamoto za wagonjwa na wageni.
5. Kufuatilia utatuzi wa malalamiko kwa kushirikiana na vitengo husika.
6. Kukusanya maoni ya wagonjwa kuhusu ubora wa huduma wanazopata.
7. Kuhakikisha usiri na faragha ya taarifa za wagonjwa wakati wote.
8. Kuorodhesha malalamiko, pongezi na maoni ya wateja na kuwasilisha taarifa kwa viongozi husika.
9. Kutambua changamoto za utoaji wa huduma na kupendekeza maboresho.
10. Kushiriki katika mafunzo ya huduma kwa wateja na shughuli za kuboresha ubora wa huduma.
11. Kufuatilia utekelezaji wa maboresho yaliyopendekezwa kutokana na maoni na malalamiko ya wateja.

12. Kuhamasisha utamaduni wa kumweka mgonjwa katikati ya huduma (patient-centred care).
13. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za huduma kwa wateja kwa msimamizi au kitengo husika.

Sifa za Mwombaji:

- Awe amehitimu wa kidato cha nne (4) au sita (6) mwenye Stashahada katika fani ya Maendeleo ya Jamii, Mawasiliano, Uhusiano au sifa zingine zinazolingana na hizo kutoka vyuo vinavyo tambuliwa na Serikali
- Muombaji awasilishe barua ya maombi pamoja na nakala za vyeti vya kidato cha nne /kidato cha sita ,vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa pamoja na nakala ya Kitambulisho cha Taifa.

Umri:

Mwombaji awe na umri kati ya miaka 25 mpaka 30.

Maombi haya yatufikie kabla ya tarehe **16/10/2026** kupitia anuani:

Mkurugenzi Mtendaji.

KCMC,

S.L.P 3010,

MOSHI.

Barua pepe: kcmcadmin@kcmc.ac.tz

